# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA RAIS - TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

## TAARIFA KWA UMMA

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU WAHITIMU WA KIDATO CHA NNE MWAKA 2023 KUFANYA MABADILIKO YA TAHASUSI ZA KIDATO CHA TANO NA KOZI ZA VYUO KWA NJIA YA MTANDAO KWENYE MFUMO WA KIELEKTRONIKI WA UCHAGUZI WA WANAFUNZI WA KIDATO CHA TANO NA VYUO MWAKA 2024.**

**Ndugu Wanahabari,**

Leo nimewaita hapa kwa ajili ya kutoa taarifa muhimu kwa wahitimu wa Kidato cha Nne mwaka 2023 kuhusu fursa ya kubadilisha machaguo ya Tahasusi za Kidato cha Tano na Kozi za Vyuo vya Ualimu, Vyuo vya Kati na Elimu ya Ufundi kwenye mfumo wa kielektroniki wa uchaguzi wa wanafunzi watakaojiunga na Kidato cha Tano na Vyuo. Ikiwa ni maandalizi ya awali ya uchaguzi wa wanafunzi watakaojiunga Kidato cha Tano na Vyuo vya Serikali Mwaka 2024.

Itakumbukwa kuwa Serikali imekuwa ikitoa fursa kwa wahitimu wa Kidato cha Nne kufanya mabadiliko ya machaguo ya Tahasusi (combination) na Kozi mbalimbali walizozichagua kupitia Fomu ya Uchaguzi (***Selform***.*)* Fursa hii huwawezesha wanafunzi kurekebisha machaguo yao kulingana na ufaulu waliopata kwenye matokeo ya Mtihani wa Kidato cha Nne yaliyotangazwa na Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA).

**Ndugu wanahabari,**

Serikali kupitia Ofisi ya Rais – TAMISEMI imekamilisha zoezi la awali la kuingiza kwenye **kanzidata** taarifa zilizo kwenye Fomu za Uchaguzi za wanafunzi kama zilivyojazwa na wanafunzi wakiwa shuleni. Aidha, napenda mtambue kuwa Mabadiliko ya Sera ya

Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la Mwaka 2023 na Mitaala ya Elimu kwa Kidato cha Tano yameanza kutekelezwa, ambapo utekelezaji huo umehusisha uanzishaji wa Tahasusi mpya 49, kutoka 16 zilizokuwepo awali hadi kufikia tahasusi 65.

Tahasusi hizo mpya zitakazoanza kutekelezwa Julai, 2024 zipo katika makundi saba (7) ambayo ni: Tahasusi za Sayansi ya Jamii; Tahasusi za Lugha; Tahasusi za Masomo ya Biashara; Tahasusi za Sayansi; Tahasusi za Michezo; Tahasusi za Sanaa; na Tahasusi za Elimu ya Dini. Orodha ya masomo na Tahasusi zitakazoanza kutekelezwa Julai, 2024 **(Rejeeni kiambatisho Na.1)**

**Ndugu wanahabari,**

Kukamilika kwa zoezi hili kunatoa fursa kwa wanafunzi kuweza kufanya mabadiliko ya machaguo/ tahasusi/ kozi kwa njia ya mtandao (online). Baada ya wanafunzi kufanya marekebisho yao, kanzidata hiyo ndiyo itakayotumika kuwachagua na kuwapangia nafasi za Kidato cha Tano na Kozi mbalimbali katika Vyuo vya Kati na vya Elimu ya Ufundi kwa kuzingatia sifa za ufaulu na machaguo yao.

**Ndugu Wanahabari,**

Ofisi ya Rais – TAMISEMI inatoa fursa kwa wahitimu wa Elimu ya Sekondari Kidato cha Nne mwaka 2023 kubadili machaguo yao ili kutoa nafasi zaidi kwa Mwanafunzi kusoma tahasusi au kozi

itakayomwandaa kuwa na utaalam stahiki katika maisha yake ya baadaye. Hii ni kutokana na ukweli kwamba wakati wa ujazaji wa fomu za machaguo ya awali, tahasusi mpya 49 hazikuwepo kwenye orodha ya machaguo na pia matokeo ya mtihani wa kuhitimu Kidato cha Nne hayakuwa yametoka kumuwezesha mwanafunzi kuweza kuwa na machaguo mazuri zaidi kulingana na ufaulu wake. Hivyo, zoezi hili litatoa fursa zaidi ya wanafunzi kuongeza machaguo na kufanya machaguo mapya ya Tahasusi na Kozi. Napenda kuwasihi wazazi/walezi kushiriki katika zoezi hili kwa kushauriana na watoto wao katika kufanya machaguo sahihi kulingana na ufaulu wao.

**Ndugu Wanahabari,**

Kwa umuhimu huo, wahitimu wote wanahimizwa kufanya marekebisho ya machaguo ya tahasusi na kozi kulingana na ufaulu wao, kwa kuingia kwenye **Mfumo wa Uchaguzi wa Wanafunzi (Student Selection MIS)** unaopatikana kupitia kiunganishi cha ***selform.tamisemi.go.tz***. Aidha, maelekezo kwa wahitimu na jinsi ya kufanya mabadiliko yanapatikana kwenye mfumo wa uchaguzi wa wanafunzi. Ili kuingia kwenye mfumo itabidi mhitimu atumie **Namba ya Mtihani wa kuhitimu Kidato cha Nne mwaka 2023**, **Jina lake la Mwisho, Mwaka wa Kuzaliwa na Alama ya Ufaulu aliyopata kwenye somo atakaloulizwa na mfumo au swali lolote atakaloulizwa.**

**Ndugu wanahabari,**

Ni matumaini yangu kuwa wahitimu wote watatumia kwa ukamilifu fursa waliyopewa ya kubadilisha Tahasusi na Kozi kulingana na ufaulu waliopata na kutumia fursa ya kuchagua tahasusi mpya zitakazoanza kufundishwa Julai, 2024. Pia wataweza kusoma tahasusi/kozi ambazo wamefaulu vizuri ama wana malengo nazo zaidi.

Zoezi la kubadilisha tahasusi na vyuo litaanza rasmi tarehe **20 Machi, 2024** hadi tarehe **30 Machi, 2024**. Wanafunzi, wazazi na walezi wanakumbushwa kushauriana kikamilifu ikiwa ni pamoja na kupata ushauri wa kitaalam na kitaaluma kabla ya kufanya mabadiliko ya tahasusi au Kozi.

Ninawasisitiza wanafunzi, wazazi/ walezi kutumia muda huo vyema ili kuepusha changamoto zinazoweza kujitokeza mara baada ya matokeo ya uchaguzi wa wanafunzi wa kujiunga na Kidato cha Tano na Vyuo kutangazwa. Ni muhimu kuzingatia muda uliotolewa wa kufanya marekebisho ili ratiba ya kuwachagua na kuwapangia shule na vyuo iweze kuendelea kwa muda uliopangwa. **Baada ya matokeo ya kujiunga na Kidato cha Tano na Vyuo kutangazwa, Ofisi haitashughulikia changamoto hizo kwa kuwa fursa ya kufanya mabadiliko hayo imeshatolewa**.

**Huduma hii ya kubadilisha tahasusi ni bure na endapo wanafunzi watapata changamoto, wawasiliane na Dawati la Huduma la Mteja kupitia barua pepe: huduma@tamisemi.go.tz au kuwasiliana moja kwa moja na Kituo cha Huduma kwa Wateja kwa simu +255 262 160 210 na +255 735 160 210. Aidha, pamoja na maelekezo hayo, kwa mwanafunzi, mzazi/mlezi atakayekuwa na suala linalohitaji maelezo au ufafanuzi zaidi aende katika Ofisi za Elimu za Mikoa na Halmashauri.**

Ahsanteni kwa kunisikiliza.

Mhe. Mohammed O. Mchengerwa, (**MB**)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS**

**(TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA)**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

## ORODHA YA TAHASUSI ZA KIDATO CHA TANO ZITAKAZOTUMIKA KUANZIA MWEZI JULY,2024

| Na. | MASOMO |
|---|---|
| | **A: TAHASUSI ZA SAYANSI YA JAMII** |
| 1 | History, Geography and Kiswahili (HGK) |
| 2 | History, Geography and English Language (HGL) |
| 3 | History, Geography and French (HGF) |
| 4 | History, Kiswahili and English Language (HKL) |
| 5 | History, Geography and Arabic (HGAr) |
| 6 | History, Geography and Chinese (HGCh) |
| 7 | History, Geography and Economics (HGE) |
| 8 | History, Geography and Fasihi ya Kiswahili (HGFa) |
| 9 | History, Geography and Literature in English (HGLi) |
| | **B: TAHASUSI ZA LUGHA** |
| 10 | Kiswahili, English Language and French (KLF) |
| 11 | Kiswahili, English Language and Arabic (KLAr) |
| 12 | Kiswahili, English Language and Chinese (KLCh) |
| 13 | Kiswahili, Arabic and Chinese (KArCh) |
| 14 | Kiswahili, Arabic and French (KArF) |

| | |
|---|---|
| 15 | English Language, French and Arabic (LFAr) |
| 16 | English Language, French and Chinese (LFCh) |
| 17 | French, Arabic and Chinese (FArCh) |
| 18 | History, English Language and French (HLF) |
| 19 | History, English Language and Arabic (HLAr) |
| 20 | History, English Language and Chinese (HLCh) |
| | **C: TAHASUSI ZA MASOMO YA BIASHARA** |
| 21 | Economics, Business Studies and Accountancy (EBuAc) |
| 22 | Economics, Geography and Mathematics (EGM) |
| 23 | Economics, Commerce and Accountancy (ECAc) |
| 24 | Economics, Computer Science and Mathematics (ECsM) |
| 25 | Business Studies, Accountancy and Computer Science (BuAcCs) |
| 26 | Business Studies, Accountancy and Mathematics (BuAcM) |
| 27 | Economics, Business Studies and Islamic Knowledge (EBuI) |
| | **D: TAHASUSI ZA SAYANSI** |
| 28 | Physics, Chemistry and Mathematics (PCM) |
| 29 | Physics, Chemistry and Biology (PCB) |
| 30 | Physics, Geography and Mathematics (PGM) |
| 31 | Chemistry, Biology and Geography (CBG) |
| 32 | Physics, Mathematics and Computer Science (PMCs) |
| 33 | Chemistry, Biology and Agriculture (CBA) |
| 34 | Chemistry, Biology and Food and Human Nutrition (CBN) |

| | |
|---|---|
| | **E: TAHASUSI ZA MICHEZO** |
| 35 | Biology, Food and Human Nutrition and Sports (BNS) |
| 36 | English Language, Music and Sports (LMS) |
| 37 | Kiswahili, Music and Sports (KMS) |
| 38 | Fasihi ya Kiswahili, Music and Sports (FaMS) |
| 39 | Literature in English, Music and Sports (LiMS) |
| 40 | French, Music and Sports (FMS) |
| 41 | Arabic, Music and Sports (ArMS) |
| | **F: TAHASUSI ZA SANAA** |
| 42 | Kiswahili, English Language and Theatre Arts G(KLT) |
| 43 | Kiswahili, French and Theatre Arts (KFT) |
| 44 | Fasihi ya Kiswahili, English Language and Theatre Arts (FaLT) |
| 45 | Kiswahili, Literature in English and Theatre Arts (KLiT) |
| 46 | Kiswahili, English Language and Music (KLM) |
| 47 | Kiswahili, French and Music (KFM) |
| 48 | Fasihi ya Kiswahili, English Language and Music (FaLM) |
| 49 | Kiswahili, Literature in English and Music (KLiM) |
| 50 | Kiswahili, English Language and Fine Art (KLFi) |

| | |
|---|---|
| 51 | Kiswahili, French and Fine Art (KFFi) |
| 52 | Fasihi ya Kiswahili, English Language and Fine Art (FaLFi) |
| 53 | Kiswahili, Literature in English and Fine Art (KLiFi) |
| 54 | Kiswahili, Textile and Garment Construction and Fine Art (KTeFi) |
| 55 | English Language, Textile and Garment Construction and Fine Art (LTeFi) |
| 56 | Arabic, Textile and Garment Construction and Fine Art (ArTeFi) |
| 57 | Chinese, Textile and Garment Construction and Fine Art (ChiTeFi) |
| | **G: TAHASUSI ZA ELIMU YA DINI** |
| 58 | Islamic Knowledge, History and Geography (IHG) |
| 59 | Divinity, History and Geography (DHG) |
| 60 | Islamic Knowledge, History and Arabic (IHAr) |
| 61 | Divinity, History and English Language (DHL) |
| 62 | Islamic Knowledge, History and English Language (IHL) |
| 63 | Divinity, History and Kiswahili (DHK) |
| 64 | Islamic Knowledge, History and Kiswahili (IHK) |
| 65 | Divinity, Kiswahili and English Language (DKL) |